Dini Yako Inakugharimu Nini?

na

Ellis Forsman

Dini Yako Inakugharimu Nini?

na

Ellis Forsman

Oktoba 15, 2011

Dini Yako Inakugharimu Nini?

2 Sam. 24:24

2 Sam. 24:24, "*Lakini mfalme akamwambia Arauna, la sivyo lakini nitavinunua kwako kwa thamani yake; wala sitamtolea BWANA Mungu wangu, sadaka za kuteketezwa nisizozigharamia, hivyo Daudi akakinunua hicho kiwanja cha kupuria na wale ng'ombe kwa shekel hamsini za fedha.*"

Wakati Fulani tunafikiria kuwa dini zetu ni sehemu ya faraja, au kama nguvu inayotuwezesha kukabiliana na majukumu na mihangaiko ya maisha. Tunaichukulia kwa mtazamo wa uwezo wa kuishi maisha ya Kikristo.

Ninawafahamu watu waliozunguka huku na huko wakitafuta magari kanisani katika sehemu za kuegeshea magari ili kuangalia kwamba ni kanisa lipi ambalo waumuni wake wamebarikiwa, alafu wanahudhuria katika makanisa hayo ili wao pia wazipate Baraka hizo.

Hatupaswi kulifikiria kwa mfumo wa kile inachogharimu, bali tunapaswa…

Hilo ndiyo somo letu sasa, Dini yako inakugharimu nini?

Mazingira ya kifungu chetu ilikuwa ni sehemu laini ya Arauna, mfalme wa Wajebusi.

Daudi alimlilia Mungu kwa kuwahesabu watu wa Israeli, na mambo matatu yalipendekezwa kama adhabu juu ya Daudi: miaka saba ya njaa; miezi mitatu ya Daudi kukabiliwa na maadui zake; au siku tatu za tauni katika nchi yake.

Daudi alipewa uchaguzi wa mambo haya matatu, lakini alisuluhisha kwa kuanguka katika mikono ya Mungu ili apate rehema.

2 Sam. 24:14, "*Naye Daudi akamwambia Gadi, nimeingia katika mashaka sana; basi sasa na tuanguke katika mkono wa BWANA; kwa kuwa rehema zake ni nyingi; wala nisianguke katika mkono wa wanadamu.*"

Hivyo Bwana akatuma tauni.

2 Sam. 24:15, "*Basi BWANA akawaletea Israeli tauni tangu asubuhi hata wakati ulioamriwa; nao wakafa watu kutoka Dani mpaka Beer-sheba sabini elfu.*"

Ili kuleta hitimisho la laana hii mbaya, Daudi aliagizwa kuinua madhabahu ambapo wanyama wangetolewa kama sadaka za kuteketezwa kwa Mungu.

Arauna alipoelewa kazi ya Daudi kwa ukarimu alimpa siyo tu eneo la kujenga dhabahu, bali pia wanyama kwa ajili ya kuteketeza na vitu vingine ambavyo vingeitajika kwa ajili ya shughuli hilo.

Lakini Daudi aliamuriwa kulipa gharama iliyokamilika.

"*Sivyo, Arauna…*"

Arauna alipenda kutoa, lakini Daudi alitamani kununua; hivyo hakupata njia rahisi ya kumtumikia Mungu.

Huduma kwa Mungu, kama inapaswa kugharimu cho chote, kama inapaswa kuwa na thamani yo yote, ni shughuli iliyo na gharama

Vitu hivyo ambazo ni za thamani kumiliki siyo rahisi kuvishinda.

Tunaonekana zaidi kushukuru vitu tunapofanya kazi kwa bidii ili kuvipata.

Elimu inagharima.

Wanafunzi waliofanya kazi ili kupata pesa zao kwa ajili ya elimu yao wameshukuru sana kuliko wale ambao elimu yao imelipwa na wazazi wao.

Gharama ya elimu kifedha ni kubwa, lakini siyo kuu. Fikiri kuhusu jukumu la mwanafunzi katika saa za masomo, kazi za darasani, na kazi za mwanafunzi.

Kuwa mkaidi katika shule au chuo ni kutupa nafasi ya mtu katika kumwandaa na changamoto ya maisha.

Ndoa inagharima.

Mafanikio hapa yanakuja tu wakati ambapo mume na mke wako tayari kulipa gharama ambayo mafanikio yanahitaji.

Siyo lengo kufikiria katika majuma machache au miezi mbele, lakini kadiri jinsi ambavyo ushirika huu unafikia ukomo, ni changamoto kwa mwanamume na mwanamke ambao siyo wabinafsi.

Ili mtu awe mkimbiaji imara lazima agharimike.

Pale ambapo uwezo wa asili ni muhimu, bado inachukua masaa na masaa ya kufanya mazoezi ili kuwa mkimbiaji mzuri katika mchezo wowote. Wale wakimbia wanaofaulu katika michezo ya Olimpiki wanatumia masaa 8 hadi 10 kila siku katika barafu tangu utoto.

Hakika, uamzi huo unawagharimu maisha ya motto wa kawaida pamoja na watoto wengine.

Kile ambacho nimekielezea katika mtazamo wa elimu, ndoa na riadha pia ni kweli katika dini zetu.

Uvivu katika dini ni zaidi ya kukosa rehema kwa Mkristo katika fani kuliko cho chote kile. Dhabihu binafsi mara zote imeonyesha agizo la Mungu.

Kujikana mwenyewe ni hitaji ambalo Kristo ameweka kwa wafuasi wake.

- Luka 9:23, "*Akawaambia wote, mtu ye yote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku anifuate.*"
- Marko 10:21, "*Yesu akamkazia macho akampenda, akamwambia umepungukiwa na neno moja. Enenda ukauze ulivyo navyo vyote, uwape maskini nawe utakuwa na hazina mbinguni; kisha njoo unifuate.*"
- Rum. 12:1, "*Basi ndugu zangu nawasihi kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu ya kumpendeza Mungu ndiyo ibada yenu yenye maana.*"

Yesu ndiye "*njia*" na "*mlango ni mwembamba na njia imesonga.*"

- Yoh. 14:6, "*Yesu akamwambia mimi ndimi njia, na kweli, na uzima, mtu haji kwa Baba ila kwa njia ya mimi.*"
- Mat. 7:14, "*Bali mlango ni mwembamba na njia imesonga iendayo uzimani, nao waoinao ni wachache.*"

Watu wachache wanatamani kutoa dhabihu. Wanataka kuzunguka duniani kote. Hii ni kweli hata katika ibada zetu.

Tuna vitu vingi vilivyoruhusiwa katika dini leo. Hii imefanya dini zetu kuonekana kuwa rahisi kwetu.

Dini yako inakugharimu nini?

Katika swala zima la fedha?

Kama umetoa kama jinsi Biblia inavyofundisha, dini yako inagharama.

- 1 Kor. 16:2, "*Siku ya kwanza ya juma kila mtu kwenu na aweke hakiba kwake kwa kadiri ya kufanikiwa kwake ili kwamba michango isifanyike hapo nitakapo kuja.*"

- 2 Kor. 9:7, "*Kila mtu na atende kama alivyokusudia moyoni mwake, si kwa huzuni wala kwa lazima, maana Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo wa ukarimu.*"

Jinsi kijana mdogo Cyrus Hamlin alivyoiweka.

Cyrus Hamlin alipokuwa na umri wa miaka kumi, mama yake akampa senti 7 ili kusheherekea siku kuu kubwa. Pesa hii ilikuwa kwa ajili ya mkate. Walikwenda kanisani kwanza, alafu baada ya hapo kijana huyu akaenda dukani kununua bidhaa. Kanisani wakati sahani ya matoleo ilipokuwa ikipitishwa, akafikiria akilini mwake, "Niweke senti 1 au 2?" akaamua aweke 2. Alafu dhamira yake ikasema: "Nini, senti 5 kwa ajili ya tumbo lako, na senti 2 kwa ajili ya Bwana?" hivyo akafiria, "4 kwa ajili ya mkate, na 4 kwa ajili ya Bwana. Sahani ilipopitishwa, aliweka senti 7, na hakuwa na cha kujali. Baadaye, mama yake akamwuliza kuhusu swala hili, na akamwelezea kilichotokea akilini mwake. Mama huyu alikuwa na machozi, na akatoa senti 7 akampa yule kijana tena ili kwamba aweze kupata chakula cha siku kuu.

Mjane maskini anatumika kama mfano unaovuvia katika kutoa dhabihu.

Marko 12:41-43, "*Naye akaketi kulielekea sanduku la hazina akatazama jinsi mkutano watiavyo mapesa katika sanduku. Matajiri wengi wakatia mengi. Akaja mjane mmoja maskini, akatia senti mbili kiasi cha nusu pesa. Akawaita wanafunzi wake, akawaambia, Amini nawaambia, huyu mjane maskini ametia zaidi kuliko wote waotia katika sanduku la hazina.*"

Mungu anawabariki wale wanaomtumikia. Kuna Baraka katika kutoa.

- Mdo. 20:33-35, "*Sikutamani fedha wala dhahabu, wala mavazi ya mtu. Ninyi wenyewe mnajua ya kuwa mikono yangu hii imetumika kwa mahitaji yangu, nay a wale waliokuwa pamoja name. katika mambo yote nimewaonyesha ya kuwa kwa kushika kazi hivi imewapasa kuwa saidia wanyonge, na kuyakumbuka maneno ya Bwana Yesu, jinsi alivyosema mwenyewe, ni heri kutoa kuliko kupokea.*"
- Mat. 6:33, "*Bali utafuteni kwanza ufalme wake na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa.*"

Kwa wakati?

Kukiwa na matendo ambayo unatakiwa ufanye katika tukio kama Mkristo, nia yako, "sina muda."?

“Nina hili na kile ambalo nataka kufanya. Sina muda na ndugu yangu.”

Wote tumetoa muda uo huo. Je siyo swali la kipaumbele? Ni kipi bora, kufanya huduma y Mungu, au kufanya kile kinachotuvutia?

Tuna siku moja tu ya kuishi; hivyo, hebu na tuishi kwa kusudi. Kila usiku ukiingia, hauta jirudia tena. Nafasi zilizo kuja nazo zote zimepita. Kama tukishindwa kutimiza yote katika hudumu kwa Mungu hatutaweza kurusi katika siku hiyo na kuishi tena. Ni kama magurudumu ya mikokoteni ya zamani; zinazosonga mbele tu na nyuma hazirudi.

Katika matumizi ya talanta zako?

Mtu akiwa mgonjwa, je unamtembelea au kumhudumia?

Wengi wetu tuna uwezo huu. Kwa nini tusiweke talanta hii katika kazi? Ilimgharimu Msamaria kumsaidia yule mgeni aliyejeruhiwa.

Watu wengine wanauwezo wa kufundisha kwa mfumo mmoja au mwingine. Umeongea na rafiki yako, jirani, mfanya kazi mwenzio, au mwanafunzi mwenzio? Kwa nini usiweke talanta hii katika kazi? Ana nafsi inayofaa kuokolewa kama ya kwako.

Hakika dini ni nini isiyogharimu cho chote?

Siyo ya kweli. Haina jina na ni ya maigizo.

Dini ya kweli uanza na unaegemea katika gharama ya fikra nyingi, kujifunza, na kuomba.

Ambapo hii inakaa lazima pia isukume mioyo katika shauku na ukarimu katika hudumu kwa Mungu.

Haikubaliki kwa Mungu.

Badala ya kuikubali, anaichukia; ni kinyume cha mapenzi yake.

Malaki 1:7-10, “*Mnatoa chakula kilichotiwa unajisi juu ya madhabahu yangu nanyi mwasema sisi tumekutia unajisi kwa jinsi gani? Kwa sababu mwasema meza ya BWANA ni kitu cha kudharauliwa. Tena mtoapo sadaka aliye kipofu si vibaya? Na mtoapo sadaka walio vilema na wagonjwa si vibaya? Haya mtolee liwali wako, je atakuwa radhi nawe? Au atakubali nafsi yako? Asema BWANA wa majeshi. Na sasa nawasii ombeni fadhili za Mungu, ili atupe neema ikiwa jambo hili limetoka katika mikono yenu; je atawakubali nafsi zenu? Asema BWANA wa majeshi. Laiti angekuwapo kwenu mtu mmoja wa kuifunga milango; msije mkawasha moto bure madhabahuni pangu, sina furaha kwenu asema BWANA wa majeshi, wala sitakubali dhabihu yo yote mikononi mwenu.*”

Hivyo basi, ni kuzaa matunda mema, sasa na baadaye.

Haimuinui na kumthibitisha muabudu. Kwa ugumu inaweza kurekebisha sahihisho ya wanadamu

Tumehakikishiwa thawabu katika kazi yetu ndani ya huduma ya Bwana

Mungu hataruhusu mtu ye yote apotee katika huduma yake kama ni mwaminifu.

- Mat. 10:42, "*Na mtu ye yote atakayemnywesha mmoja wapo wa wadogo hawa ngaa kikombe cha maji ya baridi, kwa kuwa ni mwanafunzi, amini nawaambia, haitampotea kamwe thawabu yake.*"
- 1 Kor. 15:58, "Basi ndugu zangu wapendwa mwimarike, msitikisike, makazidi sana kutenda kazi ya Bwana sikuzote kwa kuwa mwajua ya kuwa taabu yenu si bure katika Bwana."

Anatoa thawabu yenye thamani sasa kwa wale wanaotoa nguvu zao au kumtumikia. Talanta zilizotolewa katika kazi yake zitazidishwa.

- Mat. 25:29 "*Kwa maana kila mwenye kitu atapewa na kuongezewa tele; lakini asiye na kitu hata kile alicho nacho, atanyang'anywa.*"
- 2 Kor. 9:8-10, "*Na Mungu aweza kuwajaza kila neema kwa wingi, ili ninyi mkiwa na riziki za kila namna siku zote mpate kuzidi sana katika kila tendo jema; kama ilivyoandikwa, ametapanya amewapa maskini, haki yake yakaa milele. Na yeye ampaye mbegu mwenye kupanda, na mkate uwe chakula atawapa mbengu za kupanda na kuzidisha, naye ataongeza mazao ya haki yenu;*"

Thawabu yetu ni kubwa mbinguni.

- Mat. 5:12, "*Furahini na kushangilia kwa kuwa thawabu yenu ni kubwa mbinguni; kwa maana ndivyo walivyowauthi manabii waliokuwa kabla yenu.*"
- 2 Pet. 1:11, "*Maana hivi mtaruzukiwa kwa ukarimu kuingia katika ufalme wa milele wa Bwana wetu, mwokozi wetu Yesu Kristo.*"

Hitimisho

Hebu tusimpe Bwana mabaki ya muda wetu, talanta, na kipato.

Hebu tuache dini yetu itugharimu kitu.

Dini yetu inamgharim Mungu kitu.

Yoh. 3:16, "*Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.*"

Inamgharimu Kristo kitu.

2 Kor. 8:9, "*Maana mmejua neema ya Bwana wetu Yesu Kristo jinsi jinsi alivyokuwa maskini kwa ajili yenu, ingawa alikuwa tajiri, ili kwamba ninyi mpate kuwa matajiri kwa umaskini wake.*"

Kwavile, tunatakiwa kuwa tayari "*kutoa miili yetu kuwa dhabihu iliyo hai takatifu inayokubaliwa na Mungu ndiyo ibada yetu yenye maana.*"